## Wabia

Wizara ya Fedha
na Uchumi

BANK OF TANZANIA

Wizara ya Kilimo, Chakula
na Ushirika

## Watekelezaji

synovate
Research reinvented

NATIONAL BUREAU OF STATISTICS
NBS
TANZANIA
STATISTICS FOR DEVELOPMENT

Shirika la Takwimu la Taifa

FINMARK TRUST
MAKING FINANCIAL MARKETS WORK FOR THE POOR

## Mwezeshaji

FSDT

Mfuko wa Kuboresha Huduma za Kifedha Nchini

FINscope

Kwa taarifa zaidi tembelea tovuti:
http://dgroups.org/groups/FinScope-Tanzania

# FINscope 2009

# Utafiti

## Mahitaji na vikwazo katika upatikanaji wa huduma za kifedha nchini Tanzania

# Yaliyomo

| Somo | Ukurasa |
|---|---|
| Utangulizi | 1 |
| Sampuli | 2 |
| Idadi ya Watanzania | 3,4 |
| Elimu na kipato | 5,6 |
| Mpanuko wa Upatikanaji wa huduma za kifedha | 7,8,9 |
| Tofauti za Kimikoa | 10 |
| Walio nje ya Huduma za kifedha kulingana na Umri | 11 |
| Uwanda wa Fursa | 12 |
| Watumiaji wa Benki | 13 |
| Vikwazo vya kupata huduma za kifedha | 14,15 |
| Bima | 16 |
| SACCOS | 17 |
| Sekta isiyo Rasmi | 18 |
| Umuhimu wa familia na marafiki | 19 |
| Simu za Mkononi | 20 |

Taasisi ya Utafiti wa Masuala ya Uchumin na Jamii (ESRF) na Kampuni ya Ushauri wa Masuala ya Maendeleo (DPC)wameshaanza kutoa taarifa, ushauri na uchambuzi yakinifu kuhusiana na takwimu za Utafiti wa FinScope 2009.

ESRF and DPC wamebuni utaratibu utakaowezesha huduma zao kutolewa kwa pamoja kwa kuangalia makundi tofauti ya soko. Wakati ESRF inachambua taarifa za FinScope na huduma kwa sekta ya umma, taasissi za elimu ya juu na watafiti ndani ya Tanzania, DCP kwa upande wake inawaangalia watoa huduma za kifedha, mashirika yasiyo ya kiserikali na mashirika ya kimataifa

# FinScope 2009

## Utangulizi

Utafiti huu wa pili wa FinScope unaakisi hali halisi kimikoa na kitaifa, na takriban wananchi 7,680 walihojiwa. FinScope ni utafiti wa kwanza na wa aina yake unaochunguza mitazamo ya watumiaji kuhusu mahitaji na vikwazo vinavyokinza upatikanaji wa huduma za kifedha nchini.


Kitini hiki kinaeleza kwa muhtasari mambo makuu yaliyogundulika kwenye utafiti wa 2009. Taarifa nzima bado haijachambuliwa kwa kina. Inajumuisha dondoo za fursa pana kwa yeyote mwenye nia ya kuelewa tasnia ya huduma za kifedha na watumiaji wake.

Chati zote zinajumuisha watu wazima kuanzia miaka 16 na kuendelea, isipokuwa kwa chati ambazo zimetolewa ufafanuzi .


# Sampuli ya FinScope

## Sampuli yenye uwakilishi kitaifa


Sampuli ya utafiti huu iliainishwa na Idara ya Takwimu ya Taifa (NBS) na inawakilisha uwiano wa ukubwa halisi wa idadi ya Watanzania. Kitakwimu maeneo yote na mikoa inawakilishwa kiuwiano.



Chati ya Ongezeko la Watu: umri na jinsia/asilimia




Chati: Idadi ya watu Wanawake – Wanaume watu wazima




# Idadi ya Watanzania

**Sehemu kubwa ya watu wa Tanzania ni vijana ambayo inaongezeka kwa asilimia 3 kwa mwaka**

Kuna hali ya kupungua kwa idadi ya watu, hususan idadi ya wanaume, kwenye kundi la kati ya miaka 20 – 24. Kuanzia miaka 20 kwenda juu, idadi ya watu inayoongezeka sana ni ya wanawake.

**Tanzania ina asilimia 5 ya wanawake zaidi kuliko wanaume**

Mabadiliko ya mgawanyo wa kijinsia yamekuwa madogo sana ukilinganisha na mwaka 2006 ambapo mgawanyo huo ulikuwa ni 52% wanawake na 48% wanaume.

# Taarifa ya Idadi ya Watu


Mgawanyiko wa watu wa Mijini / Vijijini nchini unaendelea kubaki kama ule wa mwaka 2006: Zaidi kidogo ya robo ya watu wanaishi maeneo ya mijini, na pungufu kidogo ya robo tatu ya watu wanaishi maeneo ya vijijini.

**Wanawake wanawazidi wanaume kwa takriban watu100,000 katika maeneo ya mijini na 700,000 maeneo ya vijijini**


Chati hii inaonyesha idadi halisi ya wanaume na wanawake wanaoishi maeneo ya mijini na vijijini.

Hali halisi au utafiti unaonyesha hakuna ongezeko kubwa la wahamiaji kutoka vijijini kwenda mijini baina ya wanaume na wanawake.


## Chati ya Idadi ya Watu wa Mijini – Vijijini





## Idadi ya wakazi kulingana na makadirio ya kitaifa ya mwaka 2009 - maeneo ya Vijijini/Mke-Mme



## Kiwango cha Elimu kiliofikiwa




## Chanzo cha Kipato




# Elimu na Kipato

Elimu bado inahitaji angalizo. Elimu ya msingi imeshuka kwa asilimia 2.3 tokea 2006 ingawa elimu ya sekondari imepanda kwa silimia 4.

Hata hivyo, utafiti wa bajeti kwa nyumba (HBS) wa 2007 umeonyesha asilimia 26 ya watu kuanzia miaka 16 kwenda juu hawana elimu kabisa. Mpaka sasa hatujaangalia kwa kina mkanganyiko kati ya tafiti hizi mbili. Kama takwimu zilizoonyeshwa na HBS ni sahihi, basi hali hii inatia hofu zaidi.


**Ni asilimia 20 tu ya watu wazima wana elimu ya sekondari na kwenda juu. Huu bado ni msingi mdogo wa kuijenga jamii na uchumi ulio bora.**

Watanzania bado kwa kiwango kikubwa sana wanategemea kilimo kama chanzo kikuu cha kipato, ingawa msaada kutoka kwa ndugu na marafiki una nafasi kubwa katika kipato cha watanzania wengi. Ajira rasmi imepanda toka 4% mwaka 2006 hadi 6% mwaka 2009.


# Elimu na Kipato

Kiwango cha elimu ambacho mtu amefikia kinaonekana kuwa kigezo muhimu katika kuongeza uwezekano wa kupata huduma za fedha kutoka sekta rasmi au rasmi kiasi. Kiwango cha chini cha elimu ya mtu, kinaongeza uwezekano wa kutopata huduma za fedha kabisa.

## Uwiano kati ya kiwango cha elimu na upatikanaji wa huduma za kifedha



Mpanuko wa Huduma za fedha 2009 - 2006




*Maelezo ya sekta zilizotumika kuelezea mpanuko wa huduma za fedha yanapatikana mwisho wa kitini hiki.*

## Mpanuko wa Upatikanaji wa huduma za kifedha

Taarifa zinazotokana na Utafiti wa 2009 zinaonyesha idadi ya wale wanaopata huduma za kifedha zinazotolewa na sekta rasmi imeongezeka kwa asilimia 3.3 na wale wa rasmi kiasi pia imepanda kwa asilimia 2.2. Wale waliyo kwenye sekta isiyo rasmi wamepungua kwa asilimia 7.8.

Aidha utafiti umeonyesha kuongezeka kiasi kwa wale ambao hawapati kuduma kabisa (2.3%).

# Mpanuko wa huduma za kifedha


Matumizi ya mashine za kutolea fedha (ATM) na akaunti mpya za kuweka akiba vimesaidia katika kuleta ongezeko la watu wanaopata huduma za fedha kutoka sekta rasmi.

Kuingizwa kwa taasisi nyingine zilizo rasmi kiasi kwenye kundi la sekta rasmi katika utoaji wa huduma za kifedha kumechangia kuongezeka kwa idadi ya watu wapatao huduma za fedha katika sekta hii. Huduma hizo mpya ni pamoja na M-pesa (huduma za kutuma na kupokea fedha kupitia kampuni za simu za mkononi) na mikopo mbalimbali ya nyumba na elimu inayotolewa na serikali ambayo haikupimwa katika utafiti wa awali wa mwaka 2006.

Kushuka kwa matumizi ya sekta isiyo rasmi ni kutokana na watu kuzikataa huduma kutoka vyanzo vya fedha visivyo rasmi na kujiunga na mfumo usiyo wa kifedha.


Kiwango cha wale ambao hawapati kabisa huduma za fedha (bila kuhusisha wale wanaotegemea malipo yasiyo ya kifedha) kimeshuka kwa asilimia 1.4.

## Mpanuko wa huduma za kifedha - Kwa undani





*Maelezo ya sekta zilizotumika kuelezea mpanuko wa huduma za fedha yanapatikana mwisho wa kitini hiki.*

## Mpanuko wa huduma za fedha




## Takwimu yakinifu Mijini/Vijijini




*Maelezo ya sekta zilizotumika kuelezea mpanuko wa huduma za fedha yanapatikana mwisho wa kitini hiki.*

# Mpanuko wa huduma za kifedha

**Watu wengi katika kundi la sekta rasmi na lile la waliotengwa kabisa wanaishi kwenye maeneo ya mijini, wakati katika maeneo ya vijijini wengi wako Katika makundi ya waliotengwa kabisa, wasiotumia malipo ya kifedha na sekta isiyo rasmi.**

Ingawa ukweli ni kwamba asilimia kubwa ya wale wanaohudumiwa na sekta rasmi wako maeneo ya mijini (22.1%), maeneo hayo ndiyo yenye kundi kubwa ya wale wasiyohudumiwa kabisa (34.7%)

Wanaohudumiwa na Sekta isiyo rasmi wamegawanyika kwa kiwango sawa kati ya mijini na vijijini

Wengi wa wale wanaoangukia katika kundi linalotumia malipo yasiyo ya kifedha wako maeneo ya vijijini (29%), ambako malipo hutolewa kwa huduma au bidhaa.

Katika chati ya pili takwimu halisi zinatolewa. Kwa njia hii ni rahisi kuona uhusiano mkubwa uliopo kati ya wakazi wa mijini na wale wa vijiijini.


# Tofauti za Kimikoa

Chati hii inaonyesha mikoa minane yenye watu wengi wanaopata huduma za fedha kutoka sekta rasmi.


**Mkoa wa Kilimanjaro si tu kwamba una kiwango kikubwa cha watu wanaohudumiwa na sekta rasmi, lakini pia una kiwango cha chini kwa wale walio nje. Ajabu, Kigoma ina kiwango cha juu cha walio kwenye sekta rasmi zaidi ya Iringa au Tanga.**

Mikoa minne ya juu ni ile ambayo mtu yeyote angetarajia. Asilimia ndogo ya wale walio nje ya mfumo wa huduma za fedha mkoani Kilimanjaro imechangiwa kwa kiasi kikubwa na uwepo wa taasisi fedha ambazo ni rasmi kiasi na sekta isiyo rasmi.


Mikoa yenye zaidi ya asilimia 14 ya watu walio katika mfumo rasmi




Mikoa yenye asilimia 70 au zaidi ya wakazi walio nje ya huduma za kifedha



Chati: Idadi ya watu wasiopata huduma za fedha ki-umri kwa mwaka 2006 na 2009




## Walio nje ya huduma za kifedha kulingana na Umri

**Kwa ujumla, idadi ya wale ambao hawapati huduma za kifedha imeongezeka tokea mwaka 2006, na vijana ndiyo walioathirika zaidi. Sekta zote za umma na binafsi zinahitaji kuliangalia kwa makini zaidi kundi hili.**

Chati hii inalinganisha idadi ya wasiopata/tumia huduma za kifedha katika 2006 na 2009: "Vijana" ni wale wenye umri kuanzia miaka 16-34 na watu wazima wanaanzia miaka 35 na kuendelea.

Idadi ya vijana walio nje ya huduma ya kifedha imeongezeka kwa idadi ya watu 1.2 milioni katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita. Tofauti na watu wazima, wasiopata huduma za kifedha wame-ongezeka kwa idadi ya watu 400,000.

Katika kundi la vijana, kundi ambalo linaonekana kuongezeka zaidi ni lile la umri kati ya miaka 16 na 24.

## Wigo na mgawanyo wa utumiaji wa huduma za kifedha


**Watu wanaweka akiba zaidi kuliko kukopa au kufanyia shughuli nyingine. Idadi ya watu wanaoweka akiba ni mara nne zaidi ya watu wanaokopa.**

Mtu ambaye kwa miaka miwili iliyopita ameweka akiba kwa mali amefanya vizuri zaidi kuliko yule aliyeweka akiba kwenye benki.

**Watu wana hulka ya kuweka akiba kwa watoa huduma walio katika sekta isiyo rasmi mara saba zaidi ya wanavyofanya kwenye mabenki.**

Huduma zote za bima zinafanywa kupitia sekta rasmi, lakini katika ubadilishanaji (kwenye huduma za kifedha), kuna uwiano ulio sawa kati ya tasniya rasmi na isiyo rasmi.


Chati: Uwanda wa Fursa



## Watumiaji wa benki Mijini na Vijijini 2006-2009

| Hali halisi | Idadi | Mabadiliko |
|---|---|---|
| Wenye akaunti za benki 2006 | 1,467,815 | |
| Wenye akaunti za benki 2009 | 1,951,310 | 33% |
| | | |
| Waliowahi kuwa na akaunti 2006 | 635,792 | |
| Waliowahi kuwa na akaunti 2006 | 776,986 | 22% |
| | | |
| Ambao hawakuwa na akaunti 2006 | 19,621,136 | |
| Ambao hawakuwa na akaunti 2009 | 18,262,202 | -7% |
| | | |
| Idadi ya jumla ya watu wazima 2006 | 20,365,808 | |
| Idadi ya jumla ya watu wazima 2009 | 22,349,432 | 10% |

## Mabadiliko katika matumizi ya benki kwa watu wazima




# Watumiaji wa Benki

Kumekuwepo na ongezeko kubwa la idadi ya watu wanaotumia huduma za mabenki: Wakati idadi ya watu imeongezeka kwa asilimia 10 katika miaka mitatu iliyopita, idadi ya watu wenye akaunti za benki imeongezeka kwa asilimia 33.

Ongezeko la asilimia 22 ya idadi ya watu waliokuwa wanatumia huduma za kibenki lakini wameacha hivi sasa linatia wasiwasi na huu ni upotevu wa fursa kwa mabenki.

# Vikwazo vya kupata huduma za kifedha

**Mikopo inaonekana kana kwamba si muhimu, migumu kuipata au ni shida katika kuilipa.**

Sehemu kubwa ya watu ambao hawajawahi kuomba mkopo wanasema ni kwa kuwa wanaogopa hawatokuwa na uwezo kuilipa – ni sawa na jibu tulilolipata miaka mitatu iliyopita.

Sababu nyingine ambazo hazionyeshwi hapa ni pamoja na kutojua namna ya kuomba mkopo na jinsi ya kufikia vigezo vya kukopesheka.


**Watu wanasema hawana fedha na vikwazo ni vingi kuweza kuweka akiba au kuwekeza.**

Sehemu kubwa ya watu (26%) wanasema au hawana fedha za kuweka akiba au wanahisi wanakosa kiwango kikubwa kiasi cha kuweka akiba (hii ni inaweza kuchukuliwa kama ni hali ya kujitenga mwenyewe).


Sababu kubwa ya pili ya kukosa huduma za kuweka akiba na kuwekeza (9% ya watu) ni gharama (au kimtazamo) ni kubwa sana.

Jambo la kutia moyo ni kwamba wenye kukosa imani ni asilimia 1 tu ya watu.


## Sababu za watu kutoomba mkopo





## Sababu za kutokuweka akiba na kuwekeza



## Sababu ya kutokuwa na akaunti ya benki




## Uelewa wa Huduma za Kifedha 2009




# Vikwazo vya upatikanaji wa huduma za fedha

Watu wengi wana fedha kidogo na wanadhani kwamba mabenki yana masharti mengi na yako mbali.

Fursa na gharama za kuendesha akaunti ya benki inaweza pia kuwa kikwazo. Yeyote ambaye inambidi kusafiri ili akatumie huduma za kibenki ni lazima agharamie – gharama binafsi au muda anaotumia na gharama za usafiri.

**Kukosa uelewa na elimu ni kikwazo kikubwa katika upatkanaji wa huduma za fedha**

Kuna ufahamu mdogo na kiwango kikubwa cha kutojua juu ya huduma mbalimbali za kifedha.

Watu wengi wanasema wanaelewa mkopo ni nini, lakini chini ya asilimia 60 hawajui riba ni nini. Asilimia 60 wanasema wanajua SACCOS ni nini, lakini ni nusu yao tu wanaoelewa riba ya akiba ina maana gani.

# Bima

**Sehemu kubwa ya watu hawana huduma za bima, na pia hawaelewi faida za kuwa na bima.**


Huduma rasmi za bima zinajumuisha matibabu/afya, majengo, mikopo, magari na bima ya maisha.

Huduma za bima isiyo rasmi ni pamoja na huduma ya afya ya jamii na bima ya mazishi (kufa na kuzikana).


**Umaskini na kutokuwa na uelewa wa huduma za bima vinazuia watu kujiunga na tasnia ya bima. Unahitajika mkakati maalum wa kuieleza nadharia ya bima kwa umma mpana, na huduma zake zilenge mahitaji ya walengwa kuhamasishwa kama wataona ina umuhimu kwao.**

Suala la bima hali takiwi kuwa ndoto. Tunaweza na tunawajibika kulifanya liwe sehemu ya maisha yetu. Hususan, watu maskini wanahitaji njia rahisi na nafuu za kuokoa majanga yanayowakabili.


Bima




Sababu ya kutokata bima



## Uwanachama wa SACCOS




## SAC C O S

Takwimu hizi zinaonyesha kwamba waweka akiba kwenye SACCOS ni wengi kwa asilimia 50 zaidi ya wanaokopa/wakopaji, jambo linaloashiria kuwa kuna fedha za ziada katika vikundi mbalimbali.

## Sekta Isiyo Rasmi

**Watu wanatumia njia mbalimbali katika tasniya isiyo rasmi, ingawa vikundi vya kuweka akiba ndiyo maarufu zaidi.**

Asilimia 8.5 ni wana ROSCA na asilimia 3 tu ndiyo wana ASCA. Mpaka sasa wanahudumia watu wanaofikia 107,000 ingawa idadi inategemea kuongezeka.

Ingawa haionyeshwi katika chati hii, watu 135,000 (0.6% ya watanzania) wanatumia huduma za fedha zitolewazo na watu binafsi.


**Umaskini na kutokuwa na uelewa wa huduma hizi bado vinaendelea kuwa kikwazo kwa shughuli za sekta hii.**

Mpaka sasa asilimia 21% hawafahamu uwepo wa vikundi vya aina hii na wengine asilimia 16% hawaviamini vikundi hivyo au tu hawataki kujiunga navyo.


Vikwazo hivi vinaweza tu kuondolewa kwa kuongeza elimu ya masuala ya fedha, pamoja na kuhakikisha kwamba vikundi vya kuweka akiba na kukopa vinaanzishwa na kufuatiliwa kiutekelezaji, pia kusaidiwa katika hatua za awali ( kwa kawaida ni kwa kipindi cha mwaka mmoja hivi).




## Isiyo rasmi





Sababu za kutojiunga na kikundi cha kuweka akiba katika sekta isiyo rasmi



## Watanzania wanaoweka na kukopa kutoka kwa ndugu na jamaa




## Watanzania wanaohudumiwa na sekta isiyo rasmi na wanaweka akiba na kukopa kutoka kwa ndugu na jamaa




# Kwa kiwango gani familia na marafiki ni muhimu?

**Familia na marafiki bado wana nafasi na wachangiaji muhimu katika kutoa huduma za kifedha, ingawa takwimu za watu wanaokopa na kuhifadhi kutokana na vyanzo hivi imeshuka katika muda wa miaka mitatu iliyopita.**

Katika sekta isiyo rasmi inayohusisha mpanuko wa huduma za fedha, uwekaji wa akiba na ukopaji kutoka kwa wanafamilia na marafiki unachangia kwa kiasi kidogo tu – chini kuliko huduma hizi zinavyotolewa kwa wananchi kwa ujumla.


Utegemezi wa familia na marafiki kama chanzo cha huduma za fedha unapungua katika kundi la wale wanaohudumiwa na tasnia isiyo rasmi, hali ambayo inajitokeza kwa jamii nzima kwa ujumla. Kuanguka huku kumechangia kushuka kwa kiwango cha wale wanaohudumiwa na tasnia isiyo rasmi.

# Simu za Mkononi

## Simu za mkononi

Takriban zaidi ya nusu ya watanzania, wanaokadiriwa kufikia watu wazima millioni 13.4, wanaweza kupata huduma za simu za mikononi – hili ni ongezeko la asilimia 130 ikilinganishwa na mwaka 2006.

Kuna uwezekano mkubwa wa kutumia teknolojia hii siyo tu kwa kufikisha malipo, lakini pia kwa huduma kadhaa za kifedha, ambazo kwa pamoja zinaweza kusaidia kupanua wigo wa huduma kwa kiwango kikubwa.



## TAASISI YA UTAFITI WA MASUALA YA UCHUMI NA JAMII (ESRF)

Taasisi ya Utafiti wa Masuala ya Uchumi na Jamii (ESRF) ni huru, isiyo ya faida, taasisi isiyo ya kiserikali hapa Tanzania iliyosajiliwa mwaka 1993. Taasisi ilianzishwa kutokana na haja iliyokuwepo ya kuendeleza uwezo wa kitaasisi katika masuala ya uchambuzi wa sera na kukuza uwezo wa uendeshaji. ESRF imesajiliwa kama taasisi ya uchambuzi na utafiti ikiwa na mamlaka ya kuendesha tafiti za kijamii na kiuchumi, kujenga na kuendeleza uwezo wa nguvukazi watu na taasisi kwenye masuala ya tafiti za kiuchumi na kijamii na kutoa ushauri kwenye nyanja za maendeleo ya jamii na uchumi.

Ikiwa kama moja ya taasisi muhimu za utafiti, ESRF ilichambua taarifa na takwimu za Utafiti ya FinScope 2006 na hivi sasa imeanza uchambuzi wa Utafiti wa 2009. Itaangalia takwimu zinazohusiana na wizara, idara na mamlaka za serikali, elimu ya juu na taasisi za utafiti.
Machapisho yetu yote yanapatikana kwenye ofisi zetu za ESRF na mengine kwenye tovuti yetu. Unaweza kuchangia kwenye mijadala ya masuala ya fedha, sera, uchumi na kijamii kupitia tovuti hii. Aidha ESRF inaendesha jukwaa la majadiliano kwenye: www.taknet.or.tz

Ofisi za ESRF zipo katika Kiwanja Na. 51 Mtaa wa Uporoto, (Pembezoni mwa Barabara za Ali Hassan Mwinyi), Viunga vya Ursino
P.O Box 31226 , Dar es Salaam, Tanzania
Tel: (255-22) 2760260, 2760751/2, 2760758, Fax: (255-22) 2760062
Mobile: (255-754) 780133

Email: esrf@esrf.or.tz
Website: www.esrf.or.tz

## MSAMIATI

**MSAMIATI**
**Rasmi:** Pamoja na watu wenye akaunti au waliyo na uhusiano na tasisi za kifedha kama vile benki za bishara, benki za kijamii au kampuni za bima ambazo zinasimamiwa na mdhibiti mkuu wa taasisi za huduma za fedha.
**Rasmi nyinginezo:** Zinajumuisha watu wanaotumia huduma kutoka kwenye taasisi rasmi kama vile mifuko ya akiba ya wafanyakazi, kampuni za karadha ambazo hazisimamiwi na Benki Kuu ya Tanzania au Kamishna wa Bima.

**RASMI KIASI**
**Vyama vya Kuweka na Kukopa SACCOS:** inajumuisha watu wanaotumia huduma kutoka kwenye vikundi hivi ambavyo vimesajiliwa rasmi lakini havisimamiwi na mdhibiti mkuu wa huduma za fedha nchini.
**Rasmi Kiasi-Taasisi za Mikopo**
Inajumuisha watu wanaotumia huduma kutoka kwenye taasisi za mikopo zilizosajiliwa lakini hazisimamiwi na mdhibiti mkuu wa huduma za fedha kama vile Benki Kuu.
**Rasmi kiasi nyinginezo:** Inajumuisha watu wanaotumia huduma kutoka kwenye taasisi ambazo si SACCOS na taasisi za mikopo. Taasisi hizi zina taratibu rasmi lakini hazisimamiwi na mdhibiti wa taasisi za fedha. Kundi hili linajumuisha M-Pesa na mikopo ya serikali ya nyumba na elimu.

**SIYO RASMI**
Inajumuisha watu wanaotumia huduma zinazotolewa na taasisi zisizo rasmi. Mfano:-vikundi vya vibati, benki za vijijini (VICOBA), Vyama vya Vijiji vya Kuweka na Kukopa (VSLA), vikundi mbalimbali vya kijamii vya kuweka akiba, ndugu na marafiki, biashara ndogondogo na wakopesha fedha.

**WALIO NJE YA HUDUMA ZA KIFEDHA**
**Wasiotumia Fedha:** Inajumuisha watu wasiyopatiwa huduma na makundi yote yaliyo orodheshwa hapo juu. Kundi hili pia linajumuisha watu wanaoweka akiba na kukopa, wanaokopesha au kutoa mikopo lakini wanafanya hivyo bila ya kutumia fedha (mali kwa mali).
**Wasiohudumiwa:** Inajumuisha watu wasiyojihusisha au kupewa huduma na makundi yote yaliyoorodheshwa hapo juu.

## KAMPUNI YA USHAURI WA MASUALA YA MAENDELEO (DPC)

Ofisi za DPC ambayo ndiyo iliyoratibu tafiti za FinScope 2006 na 2009 zipo Jijini Dar es Salaam.

www.finscope.dpc-tz.com

Tovuti hiyo ina taarifa nyingi sana juu ya tafiti za FinScope, hususan juu ya Tanzania.

Aidha DCP inatoa huduma za uchambuzi wa kina na kutoa taarifa maalum kulingana na mahitaji binafsi.

Tafadhali tembelea tovuti (blogi) yetu mpya : http://finscope-at-dpc.blogspot.com. Blogi hii ni hai, inavutia na inajumuisha taarifa mpya za kumbumbukumbu kwenye mtandao.

Tunawasilisha taarifa muafaka zinazohusiana na FinScope na kukukaribisha wewe utoe maoni yako, uchangie na kubadilishana mawazo.

Unaweza kuwasiliana nasi kwa kujisajili na FinScope kwenye tovuti ya DPC kwa kutuandikia kupitia info@dpc-tz.com au kwa kutupigia simu namba +255 (0)22 260 0674.

## DGROUP TOVUTI

Kwa taarifa zaidi juu ya Tafiti za FinScope 2006 na 2009 tafadhali ingia katika jukwaa la FinScope Tanzania (dgroup):

http://dgroups.org/groups/FinScope-Tanzania

Hata hivyo hii ni tovuti kwa ajili ya wanachama waliosajiliwa tu, hivyo unakaribishwa ujiunge. Tafadhali fuatilia njia iliyoonyeshwa hapo chini ili uweze kuingia kwenye jukwaa. Utapata taarifa mpya zaidi juu ya FinScope 2009, na kufanikiwa kuingia kwenye majadiliano na wadau wenzako kuhusiano na utafiti huo. Aidha nyaraka mbalimbali ikiwa ni pamoja na makala mbalimbali, mahojiano na taarifa zilizotolewa kwa vyombo vya habari zinahifadhiwa katika tovuti hiyo ambayo inahuishwa mara kwa mara.

Kitabu cha FinScope 2006 pia kinapatikana katika tovuti hii, ambako uchambuzi wa kina uliopangiliwa kulingana na mada pia umehifadhiwa.

## MFUKO WA KUBORESHA HUDUMA ZA KIFEDHA NCHINI (FSDT)

Mfuko wa Kuboresha Huduma za Kifedha Nchini (FSDT) ndiyo uliyogharimia tafiti zote za FinScope 2006 na 2009.

Mfuko huo ulizinduliwa mwaka 2005. Hivi sasa unafadhiliwa na serikali za nchi sita za: Kanada, Uingereeza, Uholanzi, Sweden na Denmark, wakishirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Benki Kuu ya Tanzania pia inajumuishwa katika utendaji wa FSDT kwa kuwakilishwa katika ngazi ya bodi ya wakurugenzi.

Lengo kuu la FSDT ni kusaidia kuwezesha watu wengi zaidi na wenye biashara ndogo ndogo kupata huduma za kifedha hapa nchini ikitiliwa maanani kwamba asilimia 70 ya Watanzania wanaishi maeneo ya vijijini, ambao ndiyo hasa walengwa wa mfuko. Lengo hili pia lina uhusiano na Mkukuta na Mpango wa Serikali wa Kurekebisha Sekta ya Fedha nchini.

Kwa taarifa zaidi juu ya FSDT, tafadhali tembelea tovuti yetu: www.fsdt.or.tz